



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



2 Mei, 2023
SIHA

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI MILIONI 999.1 ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI KUPITIA MRADI WA BOOST

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha anawatangazia Wananchi na Wakazi wa Wilaya ya Siha kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro imepokea kiasi cha fedha Tshs. 999,100,000/=(Milioni mia tisa tisini na tisa na laki moja) kutoka Serikali Kuu, Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule za awali na Msingi kupitia mradi wa BOOST katika shule 7 (Saba) za Msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha kama zinavyoonekana katika jedwali

NA	JINA LA SHULE YA MSINGI	KATA	MRADI UTAKAO TEKELEZWA	KIASI CHA FEDHA
1	Magadini	Gararagua	Ujenzi wa shule Mpya Kijiji cha Magadini	348,500,000/=
2	Lemosho	Ndumeti	Ujenzi wa Vyumba 5 vya Madarasa na matundu 3 ya vyoo	131,300,000/=
3	Loiwang	Donyomurwa	Ujenzi wa vyumba 2 vya Madarasa ya mfano ya elimu ya awali	69,100,000/=
4	Makiwaru	Makiwaru	Ujenzi wa vyumba 5 vya Madarasa na matundu 3 ya vyoo	131,300,000/=
5	Mawasiliano	Gararagua	Ujenzi wa vyumba 4 vya Madarasa na matundu 3 ya vyoo	106,300,000/=
6	NgareMji	Ngarenairobi	Ujenzi wa Vyumba 4 vya Madarasa na matundu 3 ya vyoo	106,300,000/=
7	Tindigani Naibili(Kituo shikizi Mwinuko)	Makiwaru	Ujenzi wa vyumba 4 vya Madarasa na matundu 3 ya vyoo	106,300,000/=
JUMLA YA FEDHA				999,100,000/=

Utekelezaji wa Mradi wa BOOST unatarajia kuboresha kiwango cha elimu na kutoa fursa za upatikanaji wa elimu kwa watoto wa elimu ya awali na Msingi sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya shule za Msingi Tanzania Bara.

Imetolewa na:-

MANGALU E
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha,
5-BR Elerai- Sanya Juu, S.L.P 129, 25482 SIHA.
Simu Na: 027-2970677, Nukushi: 0272970678, Barua Pepe: ded@sihadc.go.tz.
Tovuti: www.sihadc.go.tz